Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 2 Issue 1 | [December] [2026] | [Page 23] – [Page 41]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

Falsafa ya Ubuntu katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili

Bakita Malindi[1]; Dkt. Mohamed Maguo[2]; Dkt. Anna Kyamba[3]

[1]*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere- Dar es Salaam, Tanzania*

[2,3]*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania- Dar es Salaam, Tanzania*

Corresponding author: *bakitafocus@gmail.com*

Article History:
Received: Jan 19, 2026
Accepted: : June 16,2026
Published: Oct 27 2026

Keywords: Falsafa ya Ubuntu, riwaya za kisasa za Kiswahili

This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license

Ikisiri

Makala hii inahusu falsafa ya Ubuntu katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Makala hii imelenga kubainisha vipengele mbalimbali vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Riwaya teule zilizotumika wakati wa ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake ni riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Riwaya hizi zimeteuliwa kwa kuwa ziliandikwa kati ya mwaka 2001 hadi 2005 kipindi ambacho utandawazi ulizungumziwa kwa kiasi kikubwa na wanazuoni wengi katika fasihi ya Kiswahili. Vilevile riwaya hizo teule zinaakisi vizuri hali halisi ya falsafa ya Ubuntu katika nchi za Kiafrika katika zama hizi za utandawazi. Data za makala hii zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini. Aidha, data zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli, ambapo maelezo yalitumika kuwasilisha uchambuzi wa data. Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu imetumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Matokeo ya utafiti wa makala hii yamebainisha vipengele mbalimbali vya falsafa ya Ubuntu vilivyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Halikadhalika, yameonesha kuwa riwaya za kisasa za Kiswahili zimezungumzia pia falsafa ya Ubuntu inayoendana na utandawazi katika ulimwengu huu wa sasa, ingawa kuna tafiti zinazosema falsafa ya Ubuntu imepunguka ama kuporomoka kabisa katika zama hizi za usasa (Jean, 2002; Oni, 2005).

Abstract
This article examines the philosophy of Ubuntu in contemporary Swahili novels. Its objective is to identify the various elements of Ubuntu philosophy reflected in modern Swahili literary works. The selected novels used for data collection and analysis were Babu Alipofufuka (2001) and Makuadi wa Soko Huria (2002). These novels were chosen because they were written between 2000 and 2010, a period during which globalization was widely discussed by many scholars of Swahili literature. Furthermore, the selected novels effectively portray the realities of Ubuntu philosophy in African societies during the era of globalization. The data for this article were obtained through close textual reading. The data were analyzed using an interpretive approach, whereby descriptive explanations were employed to present the findings. The Bantu Ontology Theory was used in both the analysis and presentation of the data. The findings reveal various elements of Ubuntu philosophy manifested in the selected contemporary Swahili novels. Moreover, the study shows that contemporary Swahili novels also portray a form of Ubuntu philosophy that is compatible with globalization in today's world, despite studies that argue that Ubuntu philosophy has disappeared or significantly declined in the modern era (Jean, 2002; Oni, 2005).
Keywords: Ubuntu philosophy, contemporary Swahili novels.

1.1 Utangulizi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu ili kueleza tajiriba mbalimbali za maisha ya mwanajamii (Msokile, 1993). Nao Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi inawasilisha hali, mwingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Fasihi hupokea mabadiliko kulingana na maendeleo ya jamii husika. Senkoro (2007) anasema kuwa fasihi hubadilika kulingana na mabadiliko ya jamii. Mabadiliko hayo ndiyo husababisha kuibuka kwa namna mpya ya utunzi wa tanzu mbalimbali za fasihi kama vile tamthiliya, ushairi na riwaya. Riwaya ni mojawapo ya fasihi ambayo husawiri maudhui mbalimbali yanayoenda sambamba na mabadiliko ya jamii husika. Maelezo haya yanashadidiwa na Kezilahabi (2006) kwa kueleza kuwa utanzu wa riwaya ni legelege na tepetepe, wenye kugeukageuka na kubadilika kulingana na mabadiliko ya kijamii. Sambamba na hayo, Masimo (2023) anaongezea kuwa, uandishi wa riwaya ulikuwa unapokea mabadiliko kadiri muda ulivyosonga mbele. Kwa mfano baadhi ya riwaya zilizoandikwa miaka ya 1990 na kuendelea zimebeba sura mpya ya kiutandawazi inayozitofautisha na riwaya za mwanzo zilizokuwa na sifa ya kutumia lugha yenye maadili na iliyobeba maudhui ambayo yalisawiri hali halisi ya maisha ya jamii ya wakati huo.

Kimsingi, mabadiliko mbalimbali yanaikumba jamii kama vile utandawazi ndiyo hufanya kukawa na aina tofauti tofauti za riwaya kwa mfano riwaya za kisasa.

Naye, Mutua (2022) anasema riwaya za kisasa ni riwaya ambazo kazi zake zinachanganya mbinu za kijadi na za kisasa katika uandishi wake. Anaendelea kusema kuwa, riwaya za kisasa zimekuwa ngumu kueleweka na msomaji kwa sababu ya kukosa usimulizi wa moja kwa moja au uhalisia. Riwaya hizi ni changamano, na uchangamano wake unasababishwa na ukatizwaji wa usimulizi. Kwa maana hiyo, mbinu tofauti tofauti za utunzi wa kimajaribio zimechangia pakubwa katika ukatizwaji wa usimulizi unaosababisha uchangamano uliopo katika riwaya za kisasa. Kuna tafiti zinazodai kuwa falsafa ya Ubuntu imepotea katika zama hizi za usasa kutokana na athari za utandawazi katika jamii za Kibantu (Jean, 2002; Oni, 2005), ingawa utafiti huu unadhihirisha kuwa falsafa ya Ubuntu ipo na jinsi ilivyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Kwa upande mwingine, Chachage (2002) anaunga mkono suala hili kwa kusema kuwa riwaya za kisasa kwa kiasi fulani zimezungumzia pia falsafa ya Ubuntu iliyobeba sura ya utandawazi kuendana na zama hizi za sasa. Falsafa ya Ubuntu ni fikra au mitazamo wanayoishughulikia Waafrika wenyewe au watu wengine ambao wanakubali mila na desturi za Kiafrika (Oruka (2012). Naye Samwel (2015) anasema falsafa ya Ubuntu imetokana na mila na utamaduni wa Kiafrika ambao umejengwa juu ya maslahi ya jamii zaidi ya maslahi ya mtu binafsi.

Kuna tafiti mbalimbali zilizochunguza kuhusiana na falsafa ya Ubuntu, na kubainisha kuwa falsafa ya Ubuntu imejitokeza katika riwaya teule walizozishughulikia. Baadhi ya watafiti hao ni Isack (2020), Mpalanzi (2019) na Roman (2019). Wote hawa wamechunguza kuhusiana na ujitokezaji wa falsafa ya Ubuntu katika riwaya teule za Kiswahili walizoshughulikia. Watafiti hawa walichunguza riwaya za Kiswahili zisizo za kisasa. Fikra zao ni kuwa riwaya hubeba falsafa ya Ubuntu kwa kuwa vipengele vya falsafa ya Ubuntu vinadhihirika bayana katika riwaya teule za Kiswahili, vipengele hivyo ni: utu, kazi, wema, busara, hekima na haki na usawa. Vipengele vingine ni ndoa, ukarimu, upendo, malezi, huruma hali kadhalika umoja na ushirikiano. Kutokana na kupitia kundi hili la utafiti, watafiti hawa kwa ujumla hawakuchunguza bayana falsafa ya Ubuntu katika riwaya za kisasa za Kiswahili ili kuendana na mabadiliko ya utunzi wa riwaya katika zama hizi za utandawazi.

1.2 Tatizo la Utafiti

Tafiti mbalimbali zimechunguza kuhusu ujitokezaji wa Falsafa ya Ubuntu katika riwaya za Kiswahili (Roman, 2019: Isack, 2020). Tafiti hizi zilibaini kuwa falsafa ya Ubuntu inajitokeza katika riwaya za Kiswahili. Kwa upande mwingine, kuna watafiti wanaodai kuwa majilio ya utandawazi yamevuruga na kusababisha kutoweka kwa mfumo wa awali wa maisha uliojikita kwa kufuata misingi ya falsafa

ya Ubuntu (Jean, 2002: Oni, 2005). Kutokana na hoja hizi changamani, haijabainika kikamilifu ni kwa namna gani falsafa ya Ubuntu inavyoendelezwa ndani ya muktadha wa utandawazi. Hivyo, kutokana na mkanganyiko huo, kuna haja ya kufanyika kwa utafiti huu, ili kubainisha namna ambavyo falsafa ya Ubuntu inavyojitokeza katika zama hizi za utandawazi.

1.3 Malengo ya Utafiti

Makala hii inalenga kubainisha vipengele vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

2.0 Mapitio ya Maandiko na Kiunzi chaNadharia

Maandiko ya wataalamu na watafiti mbalimbali yalitumika katika kufanikisha makala hii. Vilevile, utafiti wa makala hii uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu iliyoasisiwa mwaka 1945 na Placide Tempels, Alexis Kagame na John Mbiti

2.1 Maandiko Kuhusiana na Falsafa ya Ubuntu

Waliggo (2005) amechunguza maadili kwa watoto wa shule kutoka jamii mbalimbali za Afrika Kusini, matokeo ya uchunguzi wake yanaonesha kuwa falsafa ya Ubuntu inatoweka kwa maana kwamba watoto wengi ni watovu wa nidhamu kwa wakuu wa shule, wazazi, walimu, wazee na marafiki zao. Wengi wao wanashindwa kutimiza wajibu wao wakiwa shuleni na hata nyumbani. Kukosekana kwa maadili kwa watoto wa shule ni kwenda kinyume na taratibu za falsafa ya Ubuntu, inayosemekana kupotea katika jamii ya sasa. Utafiti wa Waliggo ni tofauti na utafiti huu kwa sababu utafiti huu umechunguza ujitokezaji wa falsafa ya Ubuntu katika riwaya za kisasa za Kiswahili katika zama hizi za utandawazi.

Mabovula (2011) amechunguza kuporomoka kwa falsafa ya Ubuntu katika jamii ya Kiafrika. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa falsafa ya Ubuntu inazidi kuporomoka siku hadi siku kutokana na changamoto mbalimbali katika jamii ya Kiafrika hususani Afrika Kusini. Miongoni mwa changamoto kuu alizozibaini ni umasikini na uhaba wa rasilimali, uhalifu, matumizi mabaya ya dawa za kulevya na mengine mengi. Utafiti wa Mabovula ni tofauti na utafiti huu, kwa sababu utafiti huu umechunguza jinsi falsafa ya Ubuntu inavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

Madzore (2024) amechunguza falsafa ya Ubuntu katika jamii mbalimbali katika makundi tofauti tofauti nchini Zimbabwe. Katika utafiti wake alichunguza ni kwa jinsi gani falsafa ya Ubuntu inajitokeza kwa vijana wa Zimbabwe. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa falsafa ya Kiafrika imekumbwa na tishio la kuporomoka,

kupotea ama kutoweka katika zama hizi za utandawazi kutokana na mwingiliano wa tamaduni za mataifa mbalimbali. Anaendelea kusema kuwa kupotea au kutoweka huko kwa maadili kumeonekana katika ngazi ya chini inayowahusu watoto na hata vijana katika makuzi yao kwa ujumla. Utafiti wa Madzore ni tofauti na utafiti huu, kwa kuwa utafiti huu umechunguza jinsi falsafa ya Ubuntu inavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili kwa kuendana na zama hizi za utandawazi

2.2 Kiunzi cha Nadharia

Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu iliyoasisiwa mwaka 1945. Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu iliasisiwa na Placide Tempels (1906-1977) na Alexis Kagame (1912-1981) na John Mbiti (1931-2019). Tempels ni mwanafalsafa na padri wa kikatoliki kutoka Ubelgiji, aliyeandika kitabu cha *Bantu Philosophy* (1959), ambacho kiliweka msingi wa Ontolojia ya Kibantu. Vilevile Tempels aliibua dhana kuu kwamba ulimwengu wa Kibantu unaeleweka kwa msingi wa *nguvu hai* kama kiini cha *uwepo*. Kwa mujibu wake, kiumbe si kitu tu, bali ni nguvu yenye uhai, na viumbe vyote vina ngazi tofauti ya nguvu hiyo. Muasisi mwingine ni Alexis Kagame, ambaye ni padri wa Kikatoliki, mwanafalsafa, mshairi na mwanahistoria kutoka Rwanda. Alijulikana kwa mchango wake mkubwa katika falsafa ya Kiafrika katika kuchambua Ontolojia ya Kibantu kupitia lugha ya Kinyarwanda. Kimsingi, alipanua hoja za Tempels na kuzifafanua kitaaluma kwa kutumia mifumo halisi ya lugha, utamaduni na mantiki za Kibantu. Haya yamedhihirika katika kitabu cha Kagame (1956) *La Philosophie Bantu – Rwandaise de Letre* pale alipochambua muundo thabiti wa lugha ya Kinyarwanda na kuonesha kuwa kuna dhana za *uwepo* katika lugha hiyo zinazoakisi Ontolojia mahususi ya Kibantu. Muasisi mwingine ni John Mbiti, Mbiti (1969) katika kitabu chake cha *African Religions and Philosophy* alieleza kuwa mtu katika fikra za Kiafrika hujulikana kupitia uhusiano wake na wengine, na ndio maana anaona kuwa msingi wa Ontolojia ya Kibantu ni "mimi niko kwa sababu sisi tuko". Vilevile, alieleza kwa kina mtazamo wa Waafrika kuhusu dini, muda na jamii. Hivyo, kwa mujibu wa Mbiti *uwepo* ni wa kijamii zaidi kuliko ubinafsi.

Kwa upande mwingine, wataalamu walioiendeleza na kuiboresha Ontolojia ya Kibantu baada ya waasisi Tempels, Kagame na Mbiti ni wengi. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na Carazzon (2010), Roberto (2014) na Reeve (2016). Kwa ujumla, watalaamu hawa wameelezea Ontolojia kuwa ni mtazamo unaohusu kuwapo kwa kitu katika dunia na kuangalia vitu katika uhalisia wake. Kimsingi, nadharia ya Ontolojia ya Kibantu ina mihimili kadhaa inayoiongoza katika uchanganuzi wa data. Mihimili hiyo imejengwa juu ya mchango wa waasisi wa

nadharia hii, wanafalsafa na wanaisimu mbalimbali waliotafiti falsafa na lugha za Kiafrika. Hata hivyo, utafiti huu uliongozwa na mihimili kadhaa ya Ontolojia ya Kibantu katika uchambuzi wa data zilizokusanywa. Mihimili hiyo ni pamoja na:

(i) Uhai kama nguvu: Kila kiumbe kina nguvu inayokifanya kiwepo. Nguvu hiyo ndiyo msingi wa uwepo.

(ii) Umoja na uhusiano: Uwepo wa kiumbe hauwezi kutenganishwa na uwepo wa vingine, maisha ni mtandao unaohusiana.

(iii) Uhusiano kati ya Mungu, mizimu na wanadamu: Kuna mtandao wa kiroho unaounganisha viumbe vyote.

Hivyo, kutokana na ufafanuzi wa nadharia hii, mtafiti aliitumia mihimili hiyo kama mwongozo wa kukusanya na kuchanganua vipengele vya falsafa ya Ubuntu vilivyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Hii ni kutokana na kwamba vipengele vya falsafa ya Ubuntu vilivyobainika vilipatika ndani ya Ontolojia ya Kibantu.

3.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu kutokana na sababu kwamba uchambuzi unahusu falsafa ya Ubuntu katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Kupitia mihimili ya Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu, makala inakusudia kubainisha vipengele vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Sampuli ya utafiti huu ni riwaya za kisasa mbili za Kiswahili, ambazo ni *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Sampuli hizi ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa, ambapo mtafiti aliteua riwaya za kisasa mbili za Kiswahili kwa sababu alibaini kuwa zinatosha kuwakilisha riwaya za kisasa zilizoandikwa kuanzia mwaka 2001 hadi 2005. Hii inatokana na ukweli kwamba sampuli haipaswi kuwa kubwa sana au finyu sana, bali inapaswa kuwa toshelevu (Garg na Kothari 2016). Aidha, data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa matini, na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli, uliotumia maelezo katika ufafanuzi wa data. Hivyo, kwa kutumia mbinu hiyo ya usomaji makini wa matini, mtafiti alikusanya vipengele mbalimbali vya falsafa ya Ubuntu vilivyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Kwa kuwa vipengele vilivyokusanywa ni vingi, katika makala hii tumechambua vipengele vitano kama sampuli katika mjadala huu ili kushadidia kile kilicholengwa katika utafiti huu.

4.0 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Uwasilishaji wa data za makala hii unahusu kuchunguza ujitokezaji wa falsafa ya ubuntu katika riwaya za kisasa za Kiswahili.

4.1 Ujitokezaji wa falasafa ya Ubuntu katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili

Lengo la utafiti wa makala hii lilikuwa ni kubainisha vipengele vya falsafa ya ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili. Katika kubainisha vipengele hivyo vya falsafa ya Ubuntu, mtafiti alitumia mbinu ya usomaji makini wa matini. Kwa kuwa swali la utafiti lilikuwa ni; Vipengele vipi vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili? Kutokana na swali hilo, matokeo ya utafiti uliozaa makala hii yamebainisha hapa chini vipengele mbalimbali vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili. Vipengele vilivyobainishwa ni upendo, adabu njema, ukarimu, huruma, kazi, ndoa, uhusiano mzuri, heshima, uvumilivu, ushirikiano, uwajibikaji, wema, usawa, busara na dini. Katika makala hii tumefafanua vipengele vitano tu, ambavyo ni ushirikiano, uwajibikaji, heshima, usawa na uhusiano mzuri kwa kuongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu:

4.1.1 Ushirikiano

Ushirikiano ni hali ya kuungana na kusaidiana katika jambo, ushirikiano ni pamoja na uelewano, changamano, tangamano, ambatano, umoja na fungamano (BAKITA, 2017). Naye, Mpangala (2007) anasema ushirikiano ni kitendo cha kuungana pamoja ili kuweza kufanya jambo fulani kwa umoja na kupata mafanikio ya jambo hilo kwa pamoja. Kwa ujumla, ushirikiano ni hali au tendo la watu wawili au zaidi kufanya kazi pamoja kwa lengo moja, kwa kusaidiana, kushirikiana mawazo, na kugawana majukumu. Aidha, ushirikiano huweza kutokea baina ya mtu na mtu, mtu na watu au watu na watu, yaweza kuwa rika moja au rika tofauti tofauti. Ushirikiano ni mojawapo ya nguzo kuu katika Ontolojia ya Kibantu. Katika mtazamo wa Mbiti (1969) kiumbe hakitazamwi kama mimi peke yangu, bali kama sehemu ya mtandao wa uhusiano unaounganisha watu, mizimu, jamii na hata maumbile. Kwa kuongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu, tumefafanua suala la ushirikiano jinsi lilivyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili:

Katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, mwandishi amesawiri ushirikiano kwa kutumia wahusika mbalimbali. Kwa mfano ushirikiano ulioneshwa pale ambapo Binti Wenga alishirikiana na wanakijiji wenzake ili wamteue mtu mmoja aweze kwenda Dodoma kupeleka kero yao bungeni. Wanakijiji kwa umoja wao walishirikiana kwa kuchangishana nauli na kumteua Binti Wenga ili akawasilishe kero zao bungeni. Vilevile ushirikiano mwingine umejitokeza pale Binti Wenga alipoamua kurudi Ruhimba pamoja na wajukuu zake waliokuwa wakiishi Bamba bay, ili waanze maisha ya kujitegemea kwa kushirikiana na wifi zake. Aliamua hivyo kwa kuwa Ruhimba kulikuwa na mashamba yao ya kulima. Haya

yanadhihirika mwandishi anaposema:

> **Data 1**
> Hatimaye, Binti Wenga alitamka, "Hapana. Sisi tunaishi Ruhimba, karibu na mjini Songea. Huko Dodoma tulikwenda kumwona mbunge wa jimbo letu."
> Angefunga safari hadi Mbamba bay ambako angekusanya kila kilichowezekana pamoja na watoto wawili wa Joshua na kurudi Ruhimba kuishi maisha ya kujitegemea kwa kushirikiana na wifi zake.
> **Chanzo: Chachage (2002: 40&111)**

Dondoo hii inaonesha jinsi ambavyo ushirikiano kama kipengele cha falsafa ya Ubuntu kilivyojitokeza kati ya Binti Wenga na wanawake wenzie, na Binti Wenga na wifi zake. Ushirikiano unajitokeza kwa namna tofauti katika maisha ya kila siku tunayoishi. Kama asemavyo Roman (2019) kuwa ushirikiano kwa jamii nyingi za Kibantu ni dhana inayojitokeza katika maisha ya kila siku, na una manufaa kwa jamii nzima. Katika jamii za Kibantu mambo mengi hufanywa kwa kushirikiana na wanajamii na sio mtu peke yake. Watu hushirikiana katika kilimo, malezi ya watoto, misiba, biashara na maisha kwa ujumla. Kwa kuongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu katika mhimili wa umoja na uhusiano, ni dhahiri kuwa uwepo na thamani ya mtu hutokana na mahusuano yake na wengine. Kwa kuweka wazi jambo hili, mwandishi ameonesha jinsi ushirikiano ulivyowainua wanakijiji wa Ruhimba, hata kupata maamuzi ya kumteua mmoja wao kupeleka kero bungeni. Hivyo, uwepo wa Binti Wenga una thamani kwa wanakijiji wote kutokana na mahusiano na ushirikiano baina yake na wanajamii, mpaka kufikia hali ya kuteuliwa kupeleka kero yao bungeni. Kwa upande mwingine, mwandishi anatoa funzo kwa jamii kuwa ushirikiano ni muhimu sana katika jamii zetu, maendeleo hupatikana kupitia ushirikiano.

4.1.2 Uwajibikaji

Uwajibikaji ni hali au tabia ya mtu kukubali na kutimiza majukumu yake katika jamii anayoishi (Mbiti, 1969). Nao, Markus & Kitayama (2010) wanasema uwajibikaji ni jambo linalomlazimu mtu kutimiza wajibu kwa ustawi wa wengine na hawezi kutenda kwa ubinafsi. Wanaongezea kuwa uwajibikaji ni msingi wa haki, utu na uongozi bora. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa uwajibikaji ni kitendo cha kujituma katika kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya manufaa yako na ya jamii kwa ujumla. Katika jamii zetu yatupasa tuwajibike na kujituma katika kufanya kazi mbalimbali. Uwajibikaji na kujituma hutokea pale ambapo mtu hufanya jambo au majukumu yake ya kila siku, kwa kujitolea bila shuruti. Kila

mtu ana wajibu wa kujituma katika kufanya kazi ili aweze kujikwamua kimaisha. Katika falsafa ya Ubuntu, uwajibikaji ni sehemu ya kuishi kwa kuzingatia utu, mshikamano na manufaa ya jamii nzima. Hii ina maana kwamba mtu hawezi kuishi peke yake bila jamii. Kwa hiyo, kila mtu anatakiwa kuwajibika kwa matendo yake mbele ya jamii. Hata hivyo, katika kuchambua suala la uwajibikaji jinsi linavyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili, tumeongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu kupitia mihimili yake kama ifuatavyo:

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, uwajibikaji umesawiriwa kwa kumtumia mhusika Zuhura Mapozi alipoonesha jinsi anavyowajibika na kujituma kwa Bwana K, akiwa na lengo la kujipatia kipato. Mwandishi amemchora Zuhura kama mhusika anayependa maendeleo kwa kujishughulisha katika kufanya kazi zake. Zuhura aliwajibika katika kazi zake, pia alibuni biashara ya kumuingizia kipato ili aweze kujikwamua kimaisha, ingawa hakuwa na pesa ya kutosha kuanzisha mradi huo wa duka. Zuhura alimwomba bwana K ili ampe msingi wa shilingi milioni sabini kwa ajili ya kuanzisha duka, Bwana K alimwahidi kumpa pesa hiyo. Haya yanadhihirika mwandishi anaposema:

> **Data 2**
> "Sasa ninapanga kuanzisha duka la peremende…Naona hii ni bidhaa muhimu kwa watoto na hata watu wazima na hakuna aliyejichoma katika biashara hii. Basi kabla mtu fulani hajaamka kuanzisha biashara hii, naona niwahi…" "Vizuri," Alijibu K.
> **Chanzo: Mohamed (2001:60)**

Nukuu hii inaonesha uwajibikaji kama kipengele cha falsafa ya Ubuntu kwa kumtumia Zuhura Mapozi jinsi alivyowajibika na kujituma katika kufanya kazi. Pia alibuni kufanya biashara ya duka la peremende kwa lengo la kumwingizia kipato. Katika kufafanua kipengele hiki, tumeongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu katika mhimili wa uwepo kama nguvu ya uhai na umoja na uhusiano. Hivyo, kupitia mhimili huu ni dhahiri kuwa, kuwajibika katika kufanya kazi kunaongeza na kuimarisha nguvu ya uhai wa kiumbe. Vilevile, kuwajibika kunajenga umoja na uhusiano kati ya mtu na jamii. Katika kuelezea suala hili, mwandishi amemtumia Zuhura Mapozi kuonesha jinsi alivyowajibika na kujituma katika kufanya kazi. Pia alibuni eneo zuri la biashara na kuona panahitajika duka la kuweka peremende na vitamu vitamu. Kimsingi, kujituma kwa Zuhura katika kufanya kazi, kunaongeza na kuimarisha uwepo wa nguvu ya uhai wake na jamii. Vilevile, kutoa huduma katika duka lake kunaimarisha umoja na uhusiano wake na jamii inayomzunguka. Kama wasemavyo Markus & Kitayama (2010) kuwa, uwajibikaji ni pamoja na kujitoa kwa ajili ya wengine.

Kama ambavyo Zuhura alivyojitolea kwa kutoa huduma ya duka katika jamii inayomzunguka kulingana na mahitaji yao. Kwa upande mwingine, kupitia kipengele hiki mwandishi anatoa funzo kwa jamii kuwa yatupasa tuwajibike na kujituma katika kufanya kazi, vilevile tubuni biashara kulingana na walengwa au wahitaji katika eneo husika.

4.1.3 Heshima

Heshima ni thamani ya utu, utukufu, daraja ya juu au kitu anachopewa mtu kama alama ya kuthaminiwa katika jamii (BAKITA, 2017). Naye, Mbiti (1969) anasema kuwa heshima ni sehemu ya msingi ya maadili ya Kiafrika na inahusiana moja kwa moja na utu wa mtu, nafasi yake katika jamii na mahusiano ya kijamii. Ramose (1999) anasema heshima ndani ya falsafa ya Ubuntu haimaanishi tu adabu au utiifu wa kijamii, bali ni kutambua na kuthibitisha utu wa mtu mwingine kama msingi wa kuwepo kwako mwenyewe. Kwa ujumla, heshima ni tabia ya kuonyesha adabu, unyenyekevu, utii, busara na uangalifu katika maneno na matendo. Heshima hutokea kwa watu wa rika zote, na hubainika kupitia maneno na matendo atendayo binadamu. Katika Ontolojia ya Kibantu, heshima haielezwi tu kama adabu ya kijamii, bali kama kanuni ya kimsingi inayolinda na kuimarisha mtandao wa uhai unaounganisha viumbe vyote. Kwa mtazamo huu kuwepo ni kuwa katika uhusiano (Mbiti, 1969). Hata hivyo, heshima ni namna ya kulinda na kuthibitisha uhusiano huo. Katika kudadavua kipengele hiki tumeongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu kupitia mihimili yake kama ifuatavyo:

Katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* mwandishi amemwonesha Fidelis kuwa ni kijana mwenye heshima katika jamii yao. Fidelis alipokutana na Binti Wenga na Mathias kwa mara ya kwanza aliwasalimia kwa heshima na kutaka kujua shida yao, ingawa hakujua kama Binti Wenga ni mama yake mkubwa. Vilevile, Mjuba naye alikuwa ni kijana mwenye heshima katika ndoa yake. Mjuba alimheshimu mkewe hata kukiri kwa Sifuni kwamba hakuweza kutoka nje ya ndoa kipindi chote alipokataliwa kufanya tendo la ndoa na mkewe, alijifananisha na mnyama fungo kwa tabia zake kuwa kila akisikia kujisaidia haja kubwa, hata kama angalikuwa umbali gani bado atarudi hadi pale ambapo amekuwa akijisaidia siku zote. Haya yamedhihirika pale mwandishi anaposema:

> **Data 3**
> Ilikuwa kama vile walidhani nisingefika kutokana na hiyo mvua kubwa iliyokuwa inaendelea kunyesha. Walisimama na kusubiri. Nilimsalimia yule mama kwanza kwa heshima zote alizostahili, kisha nikamgeukia yule bwana mdogo aliyekuwa naye, Hata kabla sijauliza kama hajambo, tayari alikuwa ameshaniwahi kwa

> "Shikamoo"
> Nadhani nimekuwa nikiamini mimi ni mwanamme wa mwanamke mmoja tu, na daima nimetamani kuwa mfano bora wa uaminifu, kama ambavyo nimetamania maisha ya uadilifu na yenye heshima.
> **Chanzo: Chachage (2002:36&208)**

Nukuu hiyo inadhihirisha jinsi heshima inavyojitokeza kwa Fidelis dhidi ya Binti Wenga na Mathias. Fidelis pamoja na kutowafahamu Binti Wenga na mjukuu wake, alionesha heshima dhidi yao. Vilevile Mjuba alikuwa na heshima kwa mkewe. Kwa ujumla, baadhi ya wahusika waliosawiri suala la heshima ni pamoja na Fidelis, Mjuba na Mathias. Kwa kuongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu katika mhimili wa uhai kama nguvu, ni wazi kuwa heshima inapodhihirika huongeza na kuimarisha nguvu ya uhai ya wahusika. Mwandishi ameonesha suala hili, kwa kumtumia Fidelis jinsi alivyokuwa na heshima kwa watu wote. Fidelis alionesha heshima kwa Binti Wenga na Mathias ingawa hakuwafahamu, na wala hakujua kama ni ndugu zake. Vilevile Mjuba ameoneshwa kuwa ni mtu mwenye heshima katika ndoa yake, ijapokuwa hawakuwa na maelewano na mkewe, lakini hakuthubutu kumsaliti mkewe. Kitendo cha kuwa na heshima kwa wahusika hawa kimeongeza na kuimarisha nguvu ya uhai baina yao. Kwa ujumla, mwandishi ametoa funzo kwa jamii kuwa heshima iwe kwa watu wote yaani bila kujali umri, hadhi na jinsia, kwa mfano wakubwa kwa wadogo, viongozi kwa wanaoongozwa na wanawake kwa wanaume.

Vilevile, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, mwandishi amesawiri suala la heshima kwa kumtumia mhusika Biye. Biye ni binti aliyekuwa anafanya kazi za nyumbani kwa K. Biye alikuwa ni binti mwenye heshima, huruma, msikivu na mvumilivu. Biye alimuheshimu K, ingawa K alionesha dharau kwa Biye, hata alipomkaripia bila sababu Biye alimuheshimu na kumjibu kwa upole. Vilevile, Biye alikuwa ni mtu mwenye heshima na huruma kwa K hata pale alipokumbwa na changamoto. K aliamriwa atoke katika nyumba ya serikali ili nyumba ije ifungwe, na jeshi lilinde kila kitu kilichoachwa pale. K hakuwa na mahala pa kwenda, alibaki kushangaa tu. Biye kwa kuwa alimheshimu na kumthamini K, alimwonea huruma, na kumwanbia waende nyumbani kwao. Matendo hayo, yanarandana na maelezo ya Mbiti (1969) anaposema kuwa heshima si jambo la mtu binafsi, bali ni matokeo ya kuishi ndani ya jamii, ambapo mtu hujifunza: kuwajali wengine, kuzingatia maslahi ya pamoja, na kuepuka matendo yanayovunja mshikamano wa kijamii. Suala la heshima linadhihirika, pale mwandishi anaposema:

Data 4

> "Biyeeeee…" kwa ukali na kelele zaidi. "Beee," aliibuka kutoka pahali fulani na kuja mbio, lakini alisita alipomwona K hali ile. Alituwama na kutupa uso chini. Lakini K hakuwa na habari ya hali yake, na wala hangejali hali aliyokuwa nayo (uk. 150).
> Biye kwa heshima alifanya hisani kubwa kumchukua K kwao. Na K akajikuta tena kwa bi. Maajuza. Lakini hakuwa wa kufahamu tena wapi yupo au nini kinatokea (uk. 164).
> **Chanzo: Mohamed (2001:150&164)**

Kupitia dondoo hiyo, kipengele cha heshima kimeoneshwa na Biye dhidi ya K. Biye alimweshimu K kama mzazi wake, hata K alipokosa pa kwenda Biye alimwambia waende kwao. Katika kudadavua kipengele hiki, tumeongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu katika mhimili wa uhai kama nguvu na umoja na uhusiano. Kupitia mhimili huu ni dhahiri kuwa kumheshimu mtu mwingine ni kutambua na kuthamini nguvu ya uhai wake. Vilevile kumheshimu mtu ni uwepo wa mtu na mtu mwingine kimahusiano. Vilevile, mwandishi amemwonesha Biye alivyokuwa na heshima kiasi kwamba hakuweza kumjibu vibaya K, ingawa alikaripiwa bila kosa, alijishusha na kujibu kwa upole. Heshima aliyoionesha Biye kwa K imeongeza na kuimarisha nguvu ya uhai wao. Kadhalika, imethibitisha utu wa Biye kwa bosi wake kupitia uhusiano waliokuwa nao. Kama asemavyo Ramose (1999) kuwa heshima ni kipengele cha msingi cha falsafa ya Ubuntu kwa kuzingatia mtazamo wa kimaadili unaotambua utu wa kila mtu kupitia uhusiano wake na wengine. Kutokana na kipengele hiki mwandishi anatoa ujumbe kuwa heshima ni kitu bora, na huondoa migongano isiyo ya lazima baina ya watu, pasipo na heshima watu hufarakana, hugombana na kutopendana. Hivyo yatupasa tuheshimiane watu wote, wakubwa kwa wadogo, wake kwa waume, na tajiri kwa masikini.

4.1.4 Usawa

Usawa ni hali ya kulingana; hali ya kutokuwa na utofauti; hali ya kuwa sawasawa (BAKITA, 2017). Naye, Roman (2019) anasema kuwa usawa ni hali ya watu wote kupata haki inayofanana kulingana na uhitaji wao. Anaendelea kusema kuwa kila mtu anapewa haki, fursa na heshima sawa bila kuzingatia tofauti yoyote. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, usawa ni hali au kanuni ya kutambua kuwa watu wote wana thamani, haki, na hadhi sawa, bila kubaguliwa kikabila, kijinsia, kidini, rangi au hali ya kiuchumi. Usawa ni kama mizani inayoweka ulinganifu wa vitu fulani. Usawa hufanya watu wote wajione wanalingana au kufanana, palipo na usawa matabaka hujitenga. Katika mtazamo wa Ontolojia ya Kibantu, usawa si tu kufanana kabisa, bali ni uwiano na uhusiano wa thamani miongoni mwa viumbe

vyote. Kimsingi, hakuna kiumbe kinachojitosheleza peke yake, bali kila kiumbe hutegemea kingine. Hivyo, suala la usawa tumelifafanua hapa chini jinsi linavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili:

Katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, usawa na haki umejitokeza pale Mzee Mrisho alipowaeleza akina Mjuba kuhusiana na jadi ya asili ya huko kwao kwamba kila kilichopatikana walikitumia kwa usawa na haki. Hivyo hakuna aliyejionesha kuwa yuko juu ya wengine, kwa mfano tajiri au masikini. Kwa asili ya jadi ya akina Mzee Mrisho waliamini kwamba utajiri wa mtu uko rohoni, na mali ilikuwa ni kitu cha kufaidi watu wote. Haya yanadhihirika mwandishi anaposema:

> **Data 5**
> Alieleza: kujionyesha katika utajiri au ufahari haikuwa jadi yao, katika asili yao ni watu walioamini kwamba utajiri ulikuwa rohoni, na mali ilikuwa ni kitu cha kufaidi watu wote kwa usawa, na ndiyo hiyo maana halisi ya sherehe.
> **Chanzo: Chachage (2002:202)**

Dondoo hiyo inadhihirisha suala la usawa pale Mzee Mrisho alipowaeleza akina Mjuba kuwa kwa asili ya pale kijijini mali ni kitu kilichofaidiwa na watu wote kwa usawa. Hapo kijijini wanaamini kwamba utajiri wa mtu uko rohoni, na mtu kujiona fahari kuliko wengine haikuwa jadi yao. Viongozi na wazee wa pale kijijini walisisitiza misingi ya usawa na haki kwa wote. Katika kafafanua kipengele hiki tumeongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu katika mhimili wa umoja na uhusiano. Hivyo, ni dhahiri kuwa kuwepo si kitu cha mtu binafsi bali ni mtandao wa mahusiano. Katika jamii ya akina Mzee Mrisho, wanajamii walikuwa na umoja na mahusiano mazuri miongoni mwao, hivyo kila walichokipata walikitumia kwa usawa. Mwandishi ameonesha suala la usawa kwa kumtumia Mzee Mrisho na wanakijiji wenzake jinsi walivyotumia pamoja na kwa usawa kile walichokizalisha. Katika jamii yao kushiriki pamoja katika shida na raha ni jambo lililopewa kipaumbele na kwa usawa. Kimsingi, wanajamii hawa walionesha ushirikiano katika majukumu ya kila siku, hali ambayo hudhihirisha uwepo wa kiumbe hauwezi kutenganishwa na uwepo wa vingine. Kama asemavyo Mbiti (1969) kuwa maisha ni mtandao wa uhusiano na ushirikiano. Mbali na hayo, mwandishi anatoa funzo kwa jamii kuwa usawa na haki ni jambo muhimu katika maisha ya mwanadamu, hivyo, yatupasa watu wote tuthaminiane na kupendana ili kuimarisha suala la usawa na haki. Usawa na haki utawafanya watu wawe wamoja na kupingana na matabaka.

4.1.5 Uhusiano Mzuri

Uhusiano mzuri ni hali ya kuwa na ufungamano mzuri au maelewano mazuri baina ya watu (BAKIZA, 2010). Naye, Ramose (1999) anasema uhusiano mzuri ni hali ya watu wawili au zaidi kushirikiana kwa njia yenye heshima, uaminifu, na msaada wa pande zote, ambapo kila mmoja anajisikia salama, kuthaminiwa na kueleweka. Kimsingi, uhusiano mzuri hushirikisha mambo mengi kama vile upendo, ushirikiano na umoja. Aidha, uhusiano mzuri hutokea endapo mtu anachukulia mahitaji ya wengine kama yake kwa kuyathamini na kuyaheshimu. Kwa mfano kiongozi atakuwa na uhusiano mzuri na wale anaowaongoza endapo atachukulia mahitaji ya anaowaongoza kama yake, yaani aweze kujali changamoto za anaowaongoza na kuweza kushirikishana kwa pamoja katika kuzitatua. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, uhusiano mzuri ni hali ya kushirikiana pamoja juu ya misingi ya heshima, uaminifu, mawasiliano ya wazi na kujali hisia za kila mmoja. Kwa mtazamo wa Ontolojia ya Kibantu, uhusiano mzuri hauangaliwi tu kama makubaliano ya kijamii, bali kama uwiano sahihi wa uhai kati ya viumbe wote. Kama asemavyo Mbiti (1969) kuwa Ontolojia ya Kibantu inaona *kuwapo* kama kitu cha kiuhusiano, yaani mtu haishi peke yake bali ndani ya mtandao wa mahusiano. Sambamba na maelezo haya, Mbiti alitoa kauli kuwa *mimi niko kwa sababu sisi tupo*, akiwa na maana kwamba utu au uwepo wa mtu mmoja, unategemea uwepo wa mahusiano yake na wengine. Wazo hili linahusiana na falsafa ya Ubuntu katika fikra za Kibantu. Aidha, uhusiano mzuri umejitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili tulizozishughulikia kama tulivyofafanua hapa chini.

Katika riwaya ya *Babu alipofufuka*, uhusiano mzuri umejitokeza pale ambapo mwandishi alipomtumia mhusika Mzuka alipokuwa akisikitishwa na uongozi wa K. K alijali maslahi yake pekee na kuwaacha anaowaongoza wakibaki na changamoto zao. Mzuka alimtokea K mara kadhaa akimwelekeza kuwa na uhusiano mzuri baina yake na awaongozaye, lakini K hakujali. Kimsingi K hakuwa na utu hata kidogo kwa jamii aliyoiongoza, kama asemavyo Mbiti (1969) kuwa utu wa mtu hujengwa kupitia mahusiano yake na jamii. Kwa ujumla maelezo haya yanadhihirika pale mwandishi anaposema:

> **Data 6**
> Yule ambaye anaweza kuingia katika shida zao na kuzama. Yule anayeweza kushuka daraja ya chini kabisa kukubali kuheshimika kwa kuwaheshimu wengine. Yule ambaye anaweza kujua maweko ya watu wengi na kujitolea kuwanyanyua ili kunyayuka kwake yeye mwenyewe kustahikike…" (uk. 80)
> **Mohamed (2001:80)**

Nukuu hii inaonesha kuwa uhusiano mzuri hutokea pale ambapo watu hushirikishana changamoto zao na kuzitatua kwa pamoja. Kwa mfano kiongozi anapochukulia changamoto za anaowaongoza na kuziweka mezani tayari kwa kuzifanyia kazi, itaonesha ana uhusiano mzuri na wenzake. Kwa kuongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu katika mhimili wenye mawazo ya Mbiti unaosema umoja na uhusiano, ni dhahiri kuwa uhusiano mzuri unaijenga jamii katika umoja. Hata hivyo, uwepo wa kiumbe hauwezi kutenganishwa na uwepo wa vingine, kutokana na kwamba maisha ni mtandao wa uhusiano na ushirikiano. Kimsingi, suala la uhusiano mzuri tumelidadavua kupitia mhusika Mzuka pale alipomsisitiza K kuwa na uhusiano mzuri na anaowaongoza. Mzuka alimwona K akiwa bega kwa bega na wageni kutoka nchi za nje, na kutowajali watu anaowaongoza. Hivyo K hakupaswa kujitenga na jamii anayoiongoza, kwa sababu uwepo wake hauwezi kutenganishwa na jamii hiyo. Hii ndiyo sababu hasa ya K kuiongoza jamii, hivyo ilipaswa tu aimarishe uhusiano wake na jamii anayoiongoza. Sambamba na maelezo hayo, Ramose (1999) anasisitiza kuwa mtu hawezi kueleweka nje ya uhusiano wake na jamii, hivyo utu wa mtu huundwa kupitia mahusiano mema ndani ya jamii yake. Kupitia kipengele hiki, mwandishi anatoa funzo kwa jamii kuwa, uhusiano mzuri ni muhimu sana katika jamii kwani wanajamii wakiwa na uhusiano mzuri huweza kushirikiana kwa umoja na kufanya maamuzi ya pamoja kwa maendeleo yao.

Vilevile katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*, uhusiano mzuri umesawiriwa kwa kuwatumia wahusika waandishi wa habari kama vile Mjuba, Sifuni na Fidelis. Wahusika hawa walifanya kazi yao ya uandishi wa habari kwa upendo na ushirikiano. Kwa upande mwingine, uhusiano mzuri umejitokeza katika ngazi ya familia kama vile kwa Fidelis na Wende, kwa wapenzi na hata marafiki. Kwa kawaida watu wenye uhusiano mzuri hufanya kazi au mambo yao kwa kushirikiana huku upendo ukitawala. Watu wenye uhusiano mzuri hufurahi kwa pamoja katika kutimiza majukumu yao ya kila siku. Suala la uhusiano mzuri limedhihirika pale mwandishi anaposema:

> **Data 7**
> Huko hakuna watu wanaoogelea. Bali saa za jioni kuna watu wengi, hususan wa jamii ya Kiasia wakitembea huko kupunga upepo. Baadhi wako katika makundi ya familia na wengine ni wapenzi, ama mke na mume, wachumba au marafiki, ili mradi ni watu wenye uhusiano mzuri.
> **Chachage: (2002:69)**

Dondoo hii inaonesha jinsi watu walivyokuwa na uhusiano katika makundi

tofauti tofauti. Kwa mfano familia ya Fidelis na Wende ilionesha uhusiano mzuri kati yao, vilevile wapenzi kama Mjuba na Sifuni walikuwa na uhusiano mzuri baina yao. Kwa kuongozwa na nadharia ya Ontolojia ya Kibantu katika mhimili wa umoja na uhusiano na uhai kama nguvu, ni dhahiri kuwa maisha ni mtandao wa uhusiano na ushirikiano, hivyo uwepo wa kiumbe hauwezi kutenganishwa na viumbe wengine. Vilevile, uhusiano mzuri huongeza na kuimarisha nguvu ya uhai. Katika kuelezea suala hili tumewatumia wahusika wanandoa, marafiki na waandishi wa habari kuonesha jinsi walivyokuwa na uhusiano mzuri wakati wakifanya kazi zao kwa pamoja. Uhusiano mzuri waliokuwa nao unadhihirisha kuwa uwepo wa mhusika hauwezi kutengana na jamii. Vilevile ushirikiano mzuri wa wahusika huimarisha mtandao wa uhusiano na huongeza nguvu ya uhai. Kwa mfano, uhusiano na ushirikiano mzuri aliokuwa nao Wende kwa mumewe Fidelis, hudhihirisha kuwa uwepo wa Wende hauwezi kutenganishwa na uwepo wa Fidelis na jamii kwa ujumla. Hali hii hutokana na kwamba maisha ni mtandao wa uhusiano mzuri na ushirikiano. Vilevile, uhusiano wao mzuri huongeza na kuimarisha nguvu ya uhai. Maelezo haya yanashadadiwa na ya Tempels (1959) anaposema kuwa uhusiano mzuri ni ule unaoongeza na kuimarisha nguvu ya uhai ya wengine, si kuipunguza. Kwa upande mwingine, mwandishi amezungumzia suala la uhusiano mzuri kwa lengo la kuelimisha jamii kuwa na uhusiano mzuri katika makundi mbalimbali na hata wakati wa kufanya kazi.

5.0 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba falsafa ya Ubuntu ipo katika enzi hizi za utandawazi. Matokeo haya yanamaanisha kuwa, ingawa kipindi hiki ni cha utandawazi lakini bado falsafa ya ubuntu ambayo ni asili ya Mwafrika inajitokeza. Aidha, matokeo haya yanatofautiana na baadhi ya tafiti zinazodai kuwa falsafa ya Ubuntu imepotea ama kuporomoka katika enzi hizi za utandawazi kutokana na athari za utandawazi (Oni, 2005; Masimo 2023). Kwa upande mwingine, matokeo haya ya utafiti yanaendana kwa kiasi fulani na utafiti uliofanywa na Roman (2019) ambaye alichunguza falsafa ya Ubuntu kwa kutumia riwaya teule zilizoandikwa kabla ya kipindi cha utandawazi. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa matokeo haya ya utafiti yanakubaliana na Nadharia ya Ontolojia ya Kibantu iliyotuongoza katika utafiti huu, ambapo tulibainisha vipengele vya falsafa ya Ubuntu katika riwaya teule za kisasa za Kiswahili, kisha tukavichambua ili kukamilisha utafiti wetu.

6.0 Hitimisho na Mapendekezo

Kwa kuhitimisha, makala hii imejadili vipengele mbalimbali vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya teule za kisasa za Kiswahilli. Mjadala wa matokeo

umebainisha vipengele vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) na *Makuadi wa Soko Huria* (2002) ni ushirikiano, uwajibikaji, heshima, usawa na uhusiano mzuri. Aidha mjadala umethibitisha kuwa katika zama hizi za usasa falsafa ya Ubuntu bado ipo, ingawa inajitokeza kwa namna inayoendana na kipindi hiki cha utandawazi.

Kadhalika, utafiti huu umetoa mchango kwa kubainisha vipengele vya falsafa ya Ubuntu vinavyojitokeza katika riwaya za kisasa za Kiswahili, jambo ambalo linathibitisha kuwa falsafa ya Ubuntu ipo hata katika kipindi hiki cha utandawazi, ingawa kuna tafiti zinakiri kutoweka kwa falsafa ya Ubuntu katika kipindi cha utandawazi. Aidha, utafiti huu unapendekeza tafiti nyingine zifanyike kuhusu ulinganisho kifani au kimaudhui katika riwaya za kisasa za Kiswahili na riwaya zilizoandikwa kabla ya utandawazi kuzungumziwa katika fasihi ya Kiswahili, yaani miaka ya 1980 kurudi nyuma. Hii itasaidia kwa wanafasihi kuweza kujua namna fani na maudhui vinavyobadilika kulingana na wakati husika

Marejeleo

BAKITA. (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

BAKIZA. (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press

Carazzon, R. (2010). *Birth of New Science: The History of Ontology from Suarez to Kant.* From www.ontology.co/history. Retrieved 6 Aug 2024. 13:10

Chachage, C. L. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Garg, G na Kothari, C. R. (2016). Research Methodology: Methods and Techniques. 3rd Edition. New Age International Publishers.

Isack, Z. K. (2020). *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula na Desturi za Mavazi*. Osaka University: Text Version Publishers.

Jean, T. (2002). *The Hidden Dimension of Globalization*. What is at stake geoculturally? Global Policy Forum. New York: ATTAC.

Kagame, A. (1956). *La Philosophie Bantu-Rwandaise de Letres*. Bruxelles: Academic Royale des Sciences Colonials.

Kezilahabi, E. (2006). Utandawazi, Kiswahili na Dhana ya Wakati. Katika S. Sewangi na J. Madumulla (wah) *Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI – 2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930 – 2005).* (kur 164-172). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mabovula, N. N. (2011). The erosion of African communal values: The reappraisal of African Ubuntu philosophy. *Inkanyiso Jnl Hum & Soc Sci,* 3(1), 38-47.

Madzore, R. (2024). Revitalising the Ubuntu philosophy in a globalizing Zimbabwe.

Journal for Educators, Teachers and Trainers, 15(3), 285-298.
Markus, H. R and Kitayama, S (2010). Cultures and selves: A cycle of mutual constitution. *Perspectives on Psychological Science*, 5(4), 420-430.
Masimo, D. B. (2023). "Mkengeuko wa Utamaduni wa Waswahili katika Riwaya ya Kiswahili zama za Utandawazi." Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa)
Mbiti, J. (1969). *African Religions and Philosophy.* New York: Praeger Publishers.
Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Mpalanzi, L. (2019). "Ujitokezaji wa Falsafa ya Kiafrika katika Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili." Tasnifu ya PhD Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa)
Mpangala, G. P. (2007). "The Role of Civil Society in the 2005 General Elections in Tanzania." katika, *Tanzania Journal of Development Studies,* 7(2), 1-18. Dar es Salaam: IDS.
Msokile, M. (1993). *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya.* Dar es Salaam: TUKI
Mutua, J. (2022). Riwaya za Kimajaribio: Burudani au Kikwazo kwa Msomaji? Mfano wa Riwaya Teule za K. W. Wamitila. *International Journal of Advanced Research (IJAR),* 10(5), 468-478
Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Oni, A. A. (2005). Globalization and Its Implications on Africa Culture and Development: Challenges for Education. *International Journal of African and African American Studies*. Volume 4, no. 2.
Oruka, H. O. (2012). *Trends in Contemporary African Philosophy*. Nairobi: Nairobi Publishers.
Ramose, M. B. (1999). *African Philosophy Through Ubuntu*. Harare, Zimbabwe: Mond Books
Reeve, C. D. C. (2016). *Aristotle: Metaphysics*. USA: Hackett Publishing Company.
Roberto, G. (2014). Kuwako na Wakati: Mipaka ya Lugha kama Hatua za Falsafa katika mashairi ya Euphrase Kezilahabi. Katika *Swahili Forum* 21. uk 76-103
Roman, A. (2019). "Ujitokezaji wa Falsafa ya Ubuntu katika riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi wa Adili na Nduguze na Siku za Watenzi Wote." Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa)
Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi.* Dar es Salaam: Meveli Publishers.
Senkoro, F. E. M. K (2007). Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe. *Jarida la Kiswahili la Isimu na Fasihi*, Na

21. Uk 78-101. Dar es Salaam: TUKI

Temples, P. (1959). *Bantu Philosophy, In the Titi Turdorancea bulletin, Presence Africaine*. Paris: Joja Press Ltd

Waliggo, J. M. (2005). Law and public morality in Africa: Legal philosophical and cultural issues. *The ALRAESA Annual Conference*. 4-8 September 2005. Uganda: Entebbe.